
# THE SACRED NAME BROADCASTER

## Mtangazaji wa Jina Takatifu

1/2025



*a publication of* ***Assemblies of Yahweh***

THE SACRED NAME BROADCASTER

An **Assemblies of Yahweh** publication.
***Assemblies of Yahweh*, *The Narrow Way Newsletter*, *The Sacred Name Broadcaster*, *The Sacred Name Broadcast*, *The Sacred Scriptures*, *The Sacred Name Telecast*, and *WMLK Radio*** *are Service Marks and Trademarks of Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507*

***January 2025***
***Volume LVI, Number 10***


# YALIYOMO


**1 *Messiah katika Agano la Kale, Sehemu ya 3***
*Ukr-sto unaamini kwamba Agano Jipya linajumuisha fundisho tofauti na Agano la Kale. Je, tunathibitishaje basi, ukweli wa Messiah?*

**6 *Viumbe vya Yahweh Vilivyoumbwa, Sehemu ya 3***
*Mwenye-enzi Yahweh aliumba madarasa manne ya viumbe ili kumtumikia Yeye. Basi tuhakikishe kwamba hatulegei kamwe katika kujitolea kwetu kama walivyofanya wengine.*

**10 *Mwelekeo wa Unabii: Mnyama Mkali***
*Waandishi kama vile Elie Wiesel na wachanganuzi wengine walitoa maoni kwamba utawala wa Nazi wa Vita vya Pili vya Dunia, kwamba ulikuwa mnyama anayemeza roho.*

**17 *Sheria ya Yahweh: Amri ya Kumi, Usitamani***
*Dekalojia inajumuisha uratibu wa Sheria za Yahweh na hujenga tabia ya kiroho ya kila mtu anayeweka maisha yake kwenye msingi huu thabiti.*







Mtangazaji wa Jina Takatifu huchapishwa kila mwezi na Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507. Uandikishaji wako umelipwa na watendakazi wenzi wenye hiari wa huduma hii ambao wanajali kwamba ujumbe huu wa wokovu unapaswa kutolewa bila malipo kwa ulimwengu wote kama shahidi kabla ya Ujio wa Pili wa Yahshua Masihi. Ingawa hakuna malipo yoyote yatakayotozwa kwenye chapisho hili, MICHANGO (yote inakatwa kodi) inakubaliwa kwa shukrani ili kusaidia kulipia gharama. Tunatumahi kuwa utashiriki katika kufanya habari hii ipatikane kwa wengine.

Nukuu zote katika The Sacred Name Broadcaster zimetolewa kwa The Sacred Scriptures, Bethel Edition, 1981, Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507, isipokuwa ikitangazwa vingenevyo. Tafsiri zote za Biblia humu, zimesahihishwa ziwe thabiti na maandishi yaliyo ya awali zaidi yanayopatikana. Nakala za The Sacred Scriptures, Bethl Edition, zinapatikana. Kwa ujumbe jinsi ya kununua kopi yako, andika kwa Assemblies of Yahweh.


© Hakimiliki 2024 Assemblies of Yahweh. Haki zote zimehifadhiwa.
Malipo ya posta ya mara kwa mara huko Reading, PA 19612 (ISSN 879320). Simu (717) 933-4518. POSTA: Tuma fomu 3579 kwa Assemblies of Yahweh, SLP C, Bethel, PA 19507.

***Mwanzilishi na Mwandishi:*** *Mzee Jacob O. Meyer*

## Jalada Letu

*Jangwa la nyikani linaonyesha uzuri usio na mwisho wa uumbaji wa Yahweh- kazi ya mikono Yake inaonyesha hekima isiyo na mwisho.* ***"Ameumba dunia kwa uweza wake, ameuthibitisha ulimwengu kwa hekima yake, na kwa ufahamu wake amezitandika mbingu…."*** *(Yeremia 51:15).*

*Wakati Yahweh alimaliza wiki ya Uumbaji, aliangalia kwa mafanikio Yake na kuhitimisha kwamba ilikuwa nzuri kabisa.* ***"Elohim akaona kila kitu alichokifanya, na tazama ni chema sana."*** *(Mwanzo 1:31a)*




***"Ee Yahweh, jinsi yalivyo mengi matendo yako! Kwa hekima umevifanya vyote pia. Dunia imejaa utajiri wako."*** *(Zaburi 104:24).*

*Kabila ya binadamu, iliyoumbwa katika sura na mfano wake, limeamuriwa kuwa kamili kama Yahweh alivyo kamili. Ingawa Yahweh alitupata katika hali yenye dhambi, anataka sisi tubadilike kutoka kuwa wenye dhambi hadi kwa mtakatifu kupitia Yahshua aliye Messiah, Mwana Wake mzaliwa wa pekee.*

*Kwa sababu hiyo, kama Yahweh anaweza kuuchukua utupu na ukiwa wa Mwanzo 1:2 na kuugeuza kwenye Paradiso, anaweza pia kufanya sawa kwetu, kwa kutakasa- watu ambao watakaribishwa kwenye Ufalme wa Yahweh wakati Yahshua anarudi.*

***"Aa! Mwenye-enzi Yahweh, tazama, wewe umeziumba mbingu na nchi, kwa uweza wako mkuu na kwa mkono wako ulionyooshwa; hapana lolote lililo gumu usiloliweza…."*** *(Yeremia 32:17).*



# Messiah katika Agano la Kale

Na Mzee Jacob O. Meyer

Kuja kwa Yahshua aliye Messiah kulitabiriwa katika mwanzo wa Maandiko Matakatifu katika Mwanzo 3:15. Hapa tunapata kifungu cha Maandiko kinachoeleze jinsi Adamu na Hawa walifanya dhambi. Waliasi dhidi ya amri (maagizo) ya Baba wa Mbinguni Yahweh. Walichukua tunda la mti wa kujua mema na kujua mabaya na kulila. Kwa sababu hiyo, kitendo hiki chenye kiburi kiliitwa dhambi na Mwenye-nguvu Yahweh akawakana Adamu na Hawa, Uumbaji Wake.

Aliwatupa nje ya bustani nzuri aliyoitayarisha kwao, na kuwatuma nje ulimwenguni kufanya njia yao wenyewe. Kabla ya kufanya hili, aliwapa chanzo cha tumaini kwa wakati ujao. Alielezea kwamba mbegu ya mwanamke mwishowe ingeponda kichwa cha nyoka. Mbegu ya mwanamke inaashiria kuelekea kwa kuja kwa Messiah, na kichwa cha nyoka kinarejelea kwa Shetani aliye Ibilisi. Kifungu cha Agano Jipya




kinachoshughulika na unabii huu kinaweza kupatikana katika Warumi 16:20. ***"Naye Elohim wa amani atamseta Shetani chini ya miguu yenu upesi. Neema ya Mfalme wetu Yahshua aliye Messiah na iwe pamoja nanyi."*** (Angalia pia Ufunuo 12:9).

Kwa sababu hiyo, tunapata hapa ahadi inayotia moyo ambayo ilifanywa katika mwanzo hasa wa uwepo wa binadamu katika Mwanzo mlango wa 3. Tunapata faraja kuangalia mbele kwa wakati ambapo Yahshua aliye Messiah kwa kweli ataponda kichwa cha nyoka katika Kuja kwake Mara ya Pili. Tayari ameonekana duniani humu, mara moja, kumwaga damu Yake- alitoa maisha Yake kuwakomboa watu Wake. Wenye dhambi wote leo wanaweza kuwa na imani katika damu aliyomwaga Yahshua aliye Messiah kufidia kwa dhambi zao. Wanaweza kuwa wamesamehewa dhambi zao kwa neema Yake na kupitia imani yao katika kitendo chake cha upatanisho. Walakini, wakati Yahshua anarudi mara ya Pili, atamzuia Adui Shetani na hatimaye, atamwangamiza milele. Kisha atawahukumu wote ambao walikataa dhabihu yake ya ukombozi. Linganisha Isaya 53 na 2 Wathesalonike 1:7-10.

Yahshua aliye Messiah alitabiriwa kote katika Maandiko ya Agano la Kale, kote kurudi nyuma kwa mwanzo hasa wa manabii. Katika Luka 24:44-48, Yahshua aliye Messiah alifungua macho na ufahamu wa wanafunzi wake, ili kwamba wangeweza kuelewa kwamba kweli alikuwa Messiah aliyetabiriwa. Alileta kwa makini ya wanafunzi wake ukweli kwamba yeye Mwenyewe ni Messiah wao, mtu anayeangaziwa katikati, katika maandiko ya Agano la Kale yanayopatikana katika Sheria ya Musa, manabii na zaburi.

Katika msururu huu, ninazungumzia juu ya somo la jinsi Messiah alitabiriwa katika Agano la Kale. Watu wengi sana kwa kweli wanaamini kwamba Biblia inaweza kutenganishwa katika maagano, katika kitabu, mlango, mstari, au hata katika neno. Walakini, kinyume chake, Biblia inajumuisha kitengo kimoja kamili. Imeunganishwa katika mawazo na kusudi. Tunapothibitisha kanuni hii ya umoja wa maandishi na kuja kwa ufahamu huu imara, basi tutafika kwa kiwango cha mafundisho safi- mafundisho

ambayo hayatasambaratika au kuthibitishwa kuwa makosa kote katika juzuu. Biblia kweli ni kitabu kilicho na mafundisho safi kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, tunapoiruhusu juzuu kuoanishwa kote.

Tunapokuja kwa ufahamu kwamba Biblia inajumuisha kitengo, basi tunaelewa kwamba Agano la Kale linafunza kiwango cha juu cha maadili. Sheria za Amri Kumi,kwa mfano, zinapaswa kutuelekeza kwa uhusiano wa karibu na Baba wetu wa Mbinguni. Katika sheria hiyo ya Amri kumi, tunapata kiwango cha haki cha maisha kilichowekwa kwa Mwabudu wa Kweli. Yahshua aliye Messiah alifunza sheria hii katika Mathayo 5:17-20. Leo tunatambua kwamba watu wengi sana wanavunja Amri Kumi. Kwanza kabisa, wanatumia jina mbaya kwa Baba wa Mbinguni. Jina la baba wa Mbinguni linapatikana katika Amri ya Kwanza, na nakala ya Kiebrania kote inathibitisha kwamba Jina lake ni Yahweh (Isaya 42:8). Amri ya Nne ni sheria nyingine inayovunjwa karibu kwa wote na watu wa nchi yetu na hata ulimwengu mzima.

Amri ya Nne inaonyesha kwamba kutakuwa na siku ambayo tutaweka takatifu. Ni siku ambayo tunamheshimu Mwenye-nguvu Yahweh, Muumba, kwa sababu ya nguvu yake ya uumbaji. Ni Aliye na Nguvu na Sababu ya Kwanza Kuu. Aliufanya ulimwengu huu kuwepo kwa sababu ulikuwa mpango wake na Yeye ndiye aliyeleta vitu vyote kuwepo. Mwenye-nguvu Yahweh, Baba wa Mbinguni, pamoja na Yahshua aliye Messiah, Mwana wake mzaliwa wa pekee, Ukuu mbinguni kwa kweli ni wahusika wa kati kwenye Biblia. Siku hii haswa ya kupumzika waliyoifanya amri kwetu kutunza, katika Agano la Kale (siku ya saba ya wiki inayoitwa kawaida Jumamosi), inabaki hitaji kwetu kutunza pia katika zama hizi za Agano Jipya.

Watu wengi leo hawaelewi kwamba kama tutatii Amri Kumi kungekuwa na kupungua zaidi kwa uhalifu. Uhalifu umekatazwa kabisa katika sheria ya Yahweh. ***"Usiue. Usizini. Usiibe. Usimshuhudie jirani yako Uongo."*** (Kutoka 20:13-16) Matendo haya ya vurugu yanaonekana kwa kawaida kila mahali katika jamii kando yetu leo. Amri za Yahweh zinatengwa na wote na kwa urahisi. Walakini, hatuwezi kutupa Biblia au kiwango cha maadili inayofunza. Kama tutafanya hivyo, tutafanya jeraha kwa jamii tunayoishi, na hata zaidi, tutafanya uharibifu kwa uongozi wa Baba wetu mbinguni.


Ni wapi tunapata Yahshua aliye Messiah, Mwokozi na Mkombozi wetu ametabiriwa katika Agano la Kale? Basi tuangalie kwa kifungu kimoja tu cha Maandishi katika Yeremia mlango wa 23, ambapo tutaanza kusoma kwa mstari wa 3-6. ***"Nami nitakusanya mabaki ya kundi langu, kutoka nchi zile zote nilizowafukuza, nami nitawalea tena mazizini mwao; nao watazaa na kuongezeka. Nami nitaweka juu yao wachungaji watakaowalisha; wala hawataona hofu tena, wala kufadhaika, wala hatapotea hata mmoja wao, asema Yahweh.***

***Tazama siku zinakuja, asema Yahweh, nitakapomchipushia Daudi Tawi la haki; naye atatawala kama mfalme, atatenda kwa hekima, naye atafanya hukumu na haki katika nchi. Katika siku zake Yuda ataokolewa, na Israeli atakaa salama, na jina lake atakaloitwa ni hili, Yahweh ni haki yetu."***

Ruhusu tuangalie karibu zaidi kwa kifungu hiki cha maandiko. Kifungu hiki kutoka kwa kalamu ya nabii Yeremia kinafunza kwamba hatimaye waliotawanyika wa Yuda wangekusanywa tena kutoka miongoni mwa mataifa. Hili bado halijafanyika. Watu wengi wanaamini kwamba taifa la Israeli leo ni utimilifu wa nabii hizi, lakini hilo sio hitimisho sahihi. Taifa ndogo la Israeli leo linao Wayahudi wachache kiliko jimbo la New York, la Marekani lililo nao. Kunao Wayahudi zaidi waliotawanyika kote katika mataifa kuliko walio Wayahudi wanaoishi katika taifa la Israeli, hili hata halijumuishi watu kutoka kabila 10 za kaskazini walioenda kwenye Utumwa wa Ashuri katika 722-21 B.C.E.

Ni nani hao watu waliotabiriwa kuwa wengi hivyo kwamba wangekuwa kama mchanga wa bahari kwa idadi? Mwenye-nguvu Yahweh anasema kwamba hatimaye, hata ingawa aliwatuma kwenye adhabu ya mahakama-kwenye utumwa, angewaita na kuwaleta tena katika Nchi Takatifu. Hiyo itakuwa siku ambayo atainua Tawi la Haki kwa Daudi na mfalme ataendelea kutawala na kufanikiwa, akifanya hukumu na haki duniani. Ni nani hilo tawi, ni nani mfalme huyo?

Mfalme aliyepangwa kutawala duniani nzima katika ufalme Mpya wa Yahweh alikuja duniani kama miaka 2,000 iliyopita. Alikuja kama mtoto mdogo aliyezaliwa mjini wa Bethelem. Alikuja kama Mwana wa binadamu wa Miriamu na Yusufu (ilivyodhaniwa), ambaye walikuwa vizazi vya Mfalme Daudi. Walakini, alizaliwa na bikira Miriamu kulingana na utabiri, lakini kwa kweli alikuwa Mwana wa Yahweh Aliye Juu. Aliishi maisha ya haki, akifunza kutawala kama mfalme. Alikuja kama mfano kufunza watu wa Yahweh jinsi ya kuishi. Tunaweza kutumia maisha Yake kama muundo kwa




***Yahshua aliye Messiah ni Tawi, mzizi kutoka kwa shina la Yese. Ni Yahshua aliye Messiah, Tawi, ambaye atatawala kama mfalme wa Israeli.***

ambao tutajengea maisha yetu.

Alikufa kwa ajili yetu, akiruhusu Mwenyewe kutundikwa mtini wa Kalvari. Damu yake ilimwagwa Kalvari. Damu hiyo na maisha haya yalipatanisha kwa dhambi za ulimwengu; yanatupatanisha mimi nawe kwa dhambi zetu. Kisha baada ya ufufuo wake, alipaa Mbinguni na ameketi kwenye mkono wa kulia wa Yahweh leo. Anasubiri kazi kutoka kwa Baba Yahweh, kutumwa arudi duniani kuchukua utawala juu ya dunia hii, kuanzisha Ufalme mpya wa Yahweh- miaka 1,000 ya utawala wa Messiah duniani.

Hii ndiyo habari ya Messiah; na utabiri unaohusiana na Yeye unaweza kupatikana katika Maandishi ya Agano la Kale. Hadithi ilitolewa kwetu ili tuweze kujenga imani yetu, ikituashiria kuelekea kwa Messiah, Mwokozi na Mkombozi wa binadamu. Iliwahamasisha binadamu wa kwanza kufuatia uasi wao, na inapswa pia kututia moyo, sisi ambao tunaishi katika mwisho wa wakati.

Wakati Mtume Paulo alitoa maoni katika 1 Wakorintho 15, kwamba alikuwa akihubiri habari njema kwao, kwamba Messiah aliishi, kufa, na alizikwa, na kufufuka siku ya tatu kulingana na Maandiko, alikuwa akielekeza wasomaji wake nyuma kwa mafundisho ya mandishi ya Agano la Kale ambayo yanao utabiri wa mambo yajayo. Yahshua aliye Messiah alitimiza unabii wa kimessiah. Alikufa- Isaya 53. Alilazwa kaburini siku tatu na kucha tatu (Yona 1:17). Katika msururu huu wa jumbe za redio, natumai kuonyesha kwa kila msikilizaji kwamba Yeye ni Messiah wa kweli, anayethibitishwa moja kwa moja kutoka Maandiko ya Agano la Kale.

Geukia kwa Yeremia 23:5, ambapo tunasoma tena, ***"Nitamchipushia Daudi Tawi***

***la haki…."*** Neno tawi katika Kiebrania ni netzer. Mji ambao unaelezea Yahshua aliye Messiah alilelewa ni Nazareti ambao unamaanisha mji wa tawi.

Awali alikuja duniani humu. Alipokuja mara ya kwanza, alikuja kama mtumishi anayeteseka. Maandiko yanafunua kwamba angekuwa Tawi kutoka kwa familia ya Daudi na uthibitisho zaidi wa ukweli kwamba angelelewa katika mji wa Nazarethi na kwamba kutoka Nazarethi (mji wa tawi) angekuja Mfalme wa Israeli.

Natumai kuwa kwa makini utasoma msururu huu wa maandishi ya ujumbe wa redio na kuendelea kugundua Maandishi mengi yaliyotolewa kwa Agano la Kale ambayo yanathibitisha Yahshua kuwa Messiah. Nukuu nyingi kutoka kwa maandishi ya Agano la Kale zinaripotiwa kuonekana katika Agano Jipya, na tunaweza zaidi kuhitimisha kwamba zinazojumuishwa katika Agano Jipya ni madokezo mengi sana ya ziada kwa maandishi ya Agano la Kale.

Ni wapi tutaenda kwa uthibitisho kwamba kweli Yahshua ni Messiah wa Agano Jipya? Hatuwezi kukataa msingi wa imani ya kimessiah, unaopatikana katika inayoitwa Agano la Kale, Biblia ya Kiebrania. Kwa kutambua umoja wa Biblia, Agano la Kale na Jipya, tunaweza kufikia kwa hatua ya mafundisho safi na ni hapo ambapo tutakutana na Messiah wa kweli wa Israeli, Mfalme wa dunia, aliyetiwa mafuta wa Yahweh.

Tutakuachia na wazo hili leo, linalopatikana katika Isaya 9:6-7. ***"Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume; na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake: naye ataitwa jina lake, Mshauri wa Ajabu, El Mwenye-nguvu, Baba wa Milele, Mfalme wa Amani. Maongeo ya enzi yake na amani hayatakuwa na Mwisho kamwe, katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake, kuuthibitisha na kuutegemeza, kwa hukumu na kwa haki tangu sasa na hata milele. Bidii ya Yahweh wa majeshi ndio itakaotenda hayo."*** Yahshua aliye Messiah alitimiza unabii huu. Tunakupatia changamoto kujithibitishia kwako na kuishi kwa ujumbe wake. SNB



YAHWEH'S SPOKESMAN

## The Relationship of the Father, Son, and Holy Spirit

*Should there be many different ch-rches, such as we see in contemporary religion? This question has concerned various ministers and theologians who have been at the center of the ecumenical movement. The question has been addressed in the discussions of many prominent religious leaders over the years. Many ch-rch members also have pondered this vexing problem, as they have attempted to locate the True Worship of the Most High described in the Bible.*

***By Elder Jacob O. Meyer***

Could it be possible that the Holy Spirit is no longer active in drawing believers into unity? Or is there an invisible body of believers scattered throughout all denominations?

You may have been concerned about the many denominations yourself as you studied your Bible and encountered references to such passages as John 17:21-24: ***21 "That they may all be one; even as you, Father, are in me, and I in you, that they also may be in us: that the world may believe that you did send me. And the glory which you have given me I have given to them; that they may be one, even as we are one; I in them, and you in me, that they may be perfected into one; that the world may know that you did send me, and loved them, even as you loved me. Father, I desire that they also whom you have given me be with me where I am, that they may behold my glory, which you have given me: for you loved me before the foundation of the world."***

When we take into consideration Ephesians 4:3-6, the point is further driven home. ***"Giving diligence to keep the unity of the Spirit in the bond of peace. There is one body, and one Spirit, even as you were also called in one hope of your calling: one Master, one faith, one baptism, one El and Father of all, who is over all, and through all, and in all."***

Don't we believe that there is only **one** Holy Spirit, which has been sent forth from the Heavenly Father into the world and should clearly be leading and guiding us all into all Truth? John 16:13 certainly confirms that the Holy Spirit was given for this purpose. But should this deep-rooted desire to incorporate all believers into one fellowship take on the form that is being promoted by the ecumenical movement, in which a super organization would include all Chr-stians, regardless of what they teach or believe? Can sound doctrine be compromised upon the altar of unity for fellowship?

It is not my purpose to reiterate the complexities of these perplexing ecumenical problems merely to exploit the differences of doctrine in nominal religion, as do a multitude of other fundamentalists. My aim is not to cause further dissension or division, or promote another religious body as an end in itself, but to show you that there are indeed conscience-satisfying answers to difficulties over doctrines other than compromise. Let me illustrate.

### A History of Division


A number of years ago several books written by a former Amishman named Joseph Yoder came into my hands. I met this man close to the end of his life, and he was indeed a remarkable person.

1

*Kitabu hiki cha kina cha kurasa 16 kinathibitisha sio tu kwamba aliye Messiah alikuja na kutimiza unabii wa Agano la Kale, lakini kwamba alikuwapo awali, na kuonyesha nafasi Yake ilikuwa ipi katika uwepo huo wa awali.*

**Omba kopi yako leo!**

Andika kwa:
**ASSEMBLIES OF YAHWEH**
**PO Box C • Bethel, PA 19507**
**www.assembliesofyahweh.com**



# Viumbe vya Yahweh Vilivyoumbwa

PART 3

Na Mzee Jacob O. Meyer

***"Kwa hiyo nawashuhudia wote siku hii ya leo, ya kuwa mimi sina hatia kwa damu ya mtu awaye yote. Kwa maana sikujiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Elohim."*** (Matendo ya Mitume 20:26-27). Nimejitolea kufunza na kuhubiri hewani, mpango mzima wa kimaandiko wa wokovu kutoka kwa Mwenye-nguvu Yahweh kupitia vyombo vya habari vya elektroniki au vya kuchapisha, katika kusanyiko la mtaani hapa Bethel, Pennsylvania, na kufunza katika taasisi yetu ya kielimu (Obadiah School of the Bible kwa washirika watu wazima wanaotaka kusoma kwa undani zaidi kwenye Maandiko Matakatifu, na Dalet School, shule ya watoto wetu). Inayojumuisha katika kuhubiri na kufunza kwa SHAURI NZIMA ya Biblia nzima, kuoanisha Maandiko Matakatifu kutoka Mwanzo hadi Ufunuo bila woga au upendeleo.

Kulingana na wanatheolojia wa kihafidhina zaidi na maprofesa, njia pekee ya kutafsiri Biblia ni kwa kuioanisha kutoka Mwanzo hadi Ufunuo. Daima nimefanya hilo! Ninaamini kwamba istilahi sawa iliyotumika katika Mwanzo wa Biblia pia inayo ufafanuzi sawa katika mwisho wa juzuu, sio utafsiri mbaya wa kibinadamu.

Tambua, pia, wakati tunageuka kwa 2Timotheo 4:2-4, kwamba maandishi yanaonyesha: ***"Lihubiri neno; uwe tayari wakati ukufaao na wakati usiokufaa; karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote***

***na mafundisho. Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia walimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo."***

Hili ndilo nimekuwa nikifanya. Nimekuwa nikihubiri Neno lililoongozwa la Yahweh, Muumba wetu, Maandiko Yake Matakatifu. Nimejaribu kuwa wa kuhimiza katika sauti na kukuonyesha jinsi haraka yanapaswa kuwa maamuzi yako kufuata Maandiko matakatifu (mafundisho ya Biblia).

Kwa sababu ni dhahiri tuko katika siku za mwisho katika kufunga zama hizi za binadamu, Shetani ameteremka juu ya ulimwengu huu katika hasira kubwa, akijua anao tu wakati mfupi. Anatumia mbinu nyingi tofauti za udanganyifu katika juhudi kushawishi ulimwengu mbali kutoka kwa hamu yoyote katika Mwenye-nguvu Yahweh.

Tunaweza gundua pia katika Yeremia 23, kwamba nabii Yeremia anawahimiza watu wake kufanya mabadiliko makubwa maishani mwao. Kumbuka kwamba Yeremia alikuwa kuhani (babake alikuwa Hilkia, kuhani Mkuu); kwa sababu hiyo, wakati alianza kuweka shinikizo kwa ukuhani; chuki mbaya ilitokea. Baadhi ya makuhani hata walipendekeza mwanamume huyu mchanga auawe.Ingewezekana namna gani huyu "wa kuanzia" mchanga aongee dhidi ya familia yake mwenyewe, dhidi ya ukuhani ulioteuliwa ambao alikuwa mshiriki?

Basi tusome tamko hili katika mstari wa 9 wa Yeremia 23. ***"Katika habari za manabii. Moyo wangu ndani yangu umevunjika [Nimevunjika moyo], mifupa yangu yote inatikisika; nimekuwa kama mtu aliye mlevi, na kama mtu aliyeshindwa na divai, kwa ajili ya Yahweh, na kwa ajili ya maneno yake matakatifu."*** Mara nyingi nahisi kwa njia sawa. "Kwa nini nazungumza kwa watu ambao masikio yao yamefungwa na mioyo yao kuwa migumu?" Wakati fulani nauliza. "Kwa nini siwezi kusema neno, au kuashiria Maandiko, ambayo yataguza mioyo, kuweka hatiani wanaosikiliza, na kuwaleta wao kwenye maarifa makubwa ya kweli?" Kwa miaka 40, nimekuwa nikihubiri Biblia nzima katika huduma ya Assemblies of Yahweh. Natumai kwamba unatafuta kuungana nasi ili kwamba utaweza kupokea zawadi ya maarifa ambayo tunayo kwako.

Endelea katika mstari 10-12, tunasoma, ***"Kwa maana nchi imejaa wazinzi…."*** Sio kweli leo? Unasikia kuhusu kitendo hiki cha dhambi kwa vitendo kila mahali na hata kinatambaa kwenye machapisho yenye sifa nzuri kwa kiasi fulani. Hata gazeti za mtaani zimechapisha nakala inayopendekeza na kuchapisha barua za kupendekeza. ***"Kwa sababu ya kuapa nchi inaomboleza; malisho ya nyikani yamekauka. Mwenendo wao ni mbaya, na nguvu zao si za haki; maana NABII NA KUHANI wote wawili wanakufuru; naam, katika nyumba yangu nimeuona uovu wao, asema Yahweh. Kwa ajili ya hayo njia yao itakuwa kwao kama mahali pa kuteleza gizani: watatelemshwa na kuanguka hapo; kwa maana nimeleta uovu juu yao, naam, mwaka wa kujiliwa kwao, asema Yahweh."***

Tunaona utimilifu wa unabii huu leo. K-nisa la ukatoliki kwa sasa linakabiliwa na tatizo kali la maadili na kashfa za unyanyasaji wa kijinsi na makuhani ambazo zinafanya habari. Walakini, sio hilo tu. Pia ni ukristo wa kawaida, kwa ujumla, ambao unateseka kutokana na machafu, uongo, mafundisho ya uongo, na uovu wa maadili. Moyo wangu unavunjika kwa sababu watu wengi hivyo wa watu wa ulimwengu ambao ni waaminifu katika kutafuta Ukweli wa kibiblia bado hawajafanya kuwasiliana na huduma hii. Pengine roho zenye dhati zinahuzunishwa na kugeuzwa mbali na matendo ya

***Kwa sababu ni dhahiri tuko katika siku za mwisho katika kufunga zama hizi za binadamu, Shetani ameteremka juu ya ulimwengu huu katika hasira kubwa, akijua anao tu wakati mfupi. Anatumia mbinu nyingi tofauti za udanganyifu katika juhudi kushawishi ulimwengu huu mbali kutoka kwa hamu yoyote katika Mwenye-nguvu Yahweh.***

uovu ambayo dini ya ulimwengu inaruhusu miongoni mwao.

Tunaendelea hapa katika mstari wa 18. ***"Maana ni nani aliyesimama katika baraza la Yahweh...."*** umekubali ushauri wa Maandiko Matakatifu? Paulo anatangaza kwamba hajashindwa kuhubiri ushauri mzima wa Yahweh (ushauri mzima)- kila kitu ambacho Yahweh amesema. ***"Hata kalifahamu*** [kufahamu kusudi la Yahweh lilikuwa lipi alipotoa Neno Lake] ***neno lake na kulisikia? Ni nani aliyelitia moyoni neno langu, na kulisikia."*** Unaweza kuangalia katika Biblia yangu na unaweza kubaini kwamba nimeweka alama juzuu sana. Nimekuwa nikisoma Biblia tangu nilipokuwa kijana, na hasa nimekuwa nikisoma kwa umakini sana na kwa dhati ujumbe wake kwa zaidi ya miaka 40. Nimelifanya hili wito na mwito wangu. Kama singekuwa kwenye redio na runinga nikihubiri ujumbe, ningekuwa bado naisoma Biblia na kuishi maisha yangu kama ninavyofanya leo, kutafuta kuishi kwa kila Neno linalotoka kinywani mwa Yahweh.

Nimekuwa nikizungumza kuhusu madarasa manne ya viumbe tofauti ambao Mwenye-nguvu Yahweh aliumba kumtumikia Yeye. Hivi karibuni tu, iliripotiwa kwenye vyombo vya habari kwamba dhehebu fulani la kidini walifanikiwa katika kutengeneza mtoto msichana. Kwa nini mtu yeyote atafute kuingilia kwa uumbaji wa Yahweh kwa njia hii? Cha kuvutia, wanadai kwa uongo kwamba wameshauriana na kiumbe kutoka anga ya nje, ambaye ameteremka chini na kuwafunulia mambo ya siri kwao.

Naamini kwamba mtu fulani kutoka anga ya nje kwa kweli amekuwa hapana kuumba mbingu na nchi. Tumepokea hadithi yote ya tukio hilo katika Biblia, sio kupitia hadithi za ajabu zinazotoka kwa watu ambao wanaangazia na kuamini mambo ya kushangaza.

Walakini, wanaonekana kujua Jina la Yahweh, na pia wanatumia Elohim. Dhehebu wanatumia Jina Yahweh Elohim, kwa sababu linapatikana katika Biblia ya Kiebrania, watu wengi hata hawashughuliki na ukweli huu. Kama nitataja kwa mtu kwamba Jina Yahweh ni muhimu, na kwamba linapaswa kutumiwa katika ibada, wengi watajibu kwamba hawajawahi kusikia Jina Yahweh, ninajibu "Bila shaka umewahi. Unafahamiana na jina la silabi moja Yah, kama katika HalleluYah (Yah-weh), au IsaYah, YeremiYah, au ObadiYah, nk." "Yah" ni silabi ya kwanza, kifupi cha kishairi, kwa ujumla ikipatikana kwenye Biblia mara 49, bila kuhesabu matukio ambapo linaonekana kama kipengele katika majina ya binadamu. Cha kusikitisha, mara nyingi Jina takatifu limetafsiriwa vibaya. Jina takatifu halijapitishwa kwa usahihi kutoka kwa Kiebrania hadi Kiingereza, kama limetafsiriwa vibaya kwa umbo mseto wa Jehova, ambalo alama za vokali za Adonai zimeongezwa kwa Jina Yahweh. Lazima tukumbuke kwamba, lazima tuwe waaminifu kabisa kama tunatafsiri Biblia. Majina yanapaswa kuvukishwa (transliterated)- kamwe sio kutafsiriwa au kubadilishwa. Majina hayapaswi kutafsiriwa, lakini yanabebwa juu kutoka lugha moja hadi nyingine. Sauti lazima zionyeshe jina asili, na zinaweza.

***Yahshua, mwana wa Yahweh, alikuja duniani humu kama binadamu na kuongea Mapenzi ya Yahweh kwa binadamu, kutuleta sisi kutoka kwa hali yetu ya dhambi hadi kwa hali ya ushirika wa karibu na Yahweh.***

Nimezungumza mara kadhaa awali juu ya darasa la kwanza la viumbe walioumbwa, makerubi. Sasa, ninaenda kuangalia kwa neno Maserafi. Darasa la tatu nimalachim, na darasa la nne ni binadamu (Adamu). Sisi ni sehemu ya darasa la nne la viumbe vilivyoumbwa. Mwenye-nguvu Yahweh ameumba madarasa matatu ya viumbe wa kiroho kumtumikia Yeye. Hao ni viumbe ambao wana mawasiliano na binadamu. ***"Hakuna mtu aliyemwona Yahweh wakati wowote; mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua."*** (Yohana 1:18). Yahshua, mwana wa Yahweh, alikuja duniani humu kama binadamu na kuongea Mapenzi ya Yahweh kwa binadamu, kutuleta sisi kutoka kwa hali yetu ya dhambi hadi kwa hali ya ushirika wa karibu na Yahweh.

Tuzingatie kwa uangalifu neno maserafi. Maserafi wanaonekana wa kufanana sana kwa makerubi. Tofauti kubwa ni kwamba wana mabawa sita badala ya manne ambayo makerubi wanayo. Makerubi walikuwa viumbe waliobeba

kiti cha enzi cha Yahweh, kama unavyokumbuka katika Ezekieli 1 na 10. Katika Isaya 6:1 tunapata: ***"Katika mwaka ule aliokufa mfalme Uzia, nilimwona Yahweh ameketi katika kiti cha enzi, kilicho juu sana na kuinuliwa sana, na pindo za vazi lake zikalijaza hekalu. Juu yake walisimama maserafi; kila mmoja alikuwana mabawa sita; kwa mawili alifunika uso wake, na kwa mawili alifunika miguu yake, na kwa mawili aliruka. Wakaitana, kila mmoja na mwenzake, wakisema, Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni Yahweh wa majeshi*** [ya Kiebrania inasema Yahweh Sebaoth, Yahweh wa Majeshi]; ***dunia yote imejaa utukufu wake. Na misingi ya vizingiti ikatikisika kwa sababu ya sauti yake aliyelia, nayo nyumba ikajaa moshi."*** Wakati alikabiliwa na utukufu wa Yahweh, Isaya alitambua kwamba ni binadamu mwenye dhambi ***"Mimi ni mtu mwenye midomo michafu,"*** anasema katika Isaya 6:5. Neno maserafi katika nakala ya Kiebrania ni #8314 katika **Strong's Exhaustive Concordance Hebrew Dictionary.** Linaelezewa kama *kuungua, hivyo ni (kwa njia ya mfano) yenye sumu (nyoka); hasa ya seraph au kiumbe wa kiishara (kutoka kwa rangi ya shaba).* Likionekana katika Hesabu 21:6-8 ni maelezo ya nyoka ambayo Musa aliambiwa abandike juu ya nguzo. Wakati watu wataiangalia na kutambua nyoka huyu, wangeweza kutambua ni kutoka wapi shida zao zilitoka. Zilitoka kwa nyoka mkubwa (Ufunuo 12:9), ambaye alikuwa Shetani Ibilisi. Basi na tuelewe hilo, iwapo hujawahi kusoma somo hili, hili sio Caduceus inayoonekana kwenye nembo ya daktari. Hii ni kitu tofauti. Kwanza kabisa, nyoka hapa amebandikwa kwa nguzo, sio msalaba, kama Wakrsto wanavyolionyesha. Caduceus ilitokea kwa usuli wa upagani, bila shaka, kutoka kwa ibada ya Aesculapius wa Ugiriki ya kale. Kwa nini ulimwengu umejawa hivyo na ibada ambayo inaingiza ishara hizi zilizokataliwa za upagani? Hatuwezi kuamini kwamba ishara, ambazo kwa wakati mmoja zilihusiana kwa ibada ya upagani, sasa zimetakaswa kwa matumizi takatifu.

Hapa tunapata viumbe waliona mabawa sita (maserafi) ambao waliumbwa na Mwenye-nguvu Yahweh. Tunaweza zingatia maandishi fulani ya ziada kwa mfano Kumbukumbu la Torati 8:15, ambapo inasema, ***"Aliyekuongoza katika jangwa lile kubwa lenye kitisho, lenye nyoka za moto na nge, nchi ya kiu isiokuwa na maji; aliyekutolea maji katika mwamba mgumu."*** Kama nilivyoonyesha kwa kusanyiko hapa Betheli, Pennsylvania, katika ujumbe wa hivi karibuni, Musa aliamuriwa kuchukua idadi ya wazee na kuenda Sinai. Musa kisha aliambiwa aupige mwamba kwa fimbo yake na maji yakabubujika kutoka Horeb (au Sinai) kutelemka hadi kwa kambi ya Israeli katika mto. Pengine, maili 10 mbali. Haya ni matukio ya kimiujiza! Sayansi inajaribu kutafsiri miujiza hizi katika hisia ya kidunia, lakini inashindwa kuifanya. Kunazo fikra kubwa na matukio makubwa unaposoma Maandiko Matakatifu.

Katika Ufunuo 4:6 tunaambiwa, ***"Na mbele ya kile kiti cha enzi kulikuwa na mfano wa bahari ya kioo, kama bilauri; na katikati ya kile kiti cha enzi, na pande zake zote za kile kiti, walikuwako viumbe, wamejaa macho mbele na nyuma wenye uhai wanne."*** Hilo ndilo pia tunagundua katika vifungu vingine. *Makerubi* hawa na Maserafi wanaitwa "Viumbe hai." Neno hapa ni *zoe* katika Kigiriki. ***"Na huyo mwenye uhai wa kwanza alikuwa mfano wa simba, na kiumbe wa pili alikuwa mfano wa ndama, na kiumbe wa tatu alikuwa na uso kama uso wa mwanadamu, na kiumbe wanne alikuwa mfano wa tai arukaye*** (au hata nyoka).**"** Weka akilini kwamba kwenye bendera ya kila kabila ya Israeli katika kambi zao, tunatambua ishara hizi zikionekana kwenye bendera za kabila nne zinazoongoza, zilizokaa katika pande nne za kambi. Kwa hivyo, ni wazi kwamba Yahweh aliweka makerubi katika bustani la Edeni kuweka Adamu na Hawa nje ya bustani. Sasa, anawatumia kuleta tena Kwake vizazi vya Adamu na Hawa, kutoka kwa dhambi, hadi kwa wokovu

Hatimaye, kunao viumbe wengine hai (viumbe wa kiroho) ambao waliumbwa kwa huduma ya Yahweh, na waliitwa tu *malachim (ma'alach)*, #4397 katika **Strong's Concordance.** Neno hili linakuja kutoka kwa mzizi usiotumika kumaanisha, *kutumwa kama naibu, mjumbe haswa wa [Yahweh], hilo ni, malaika (pia nabii, kuhani au mwalimu).* Neno la mzizi linaonekana pia katika Kiiolojia na Kiarabu, lakini halithibitishwi hivyo katika lugha ya Kiebrania. Neno sawa katika maandishi ya Kigiriki ya Agano Jipya ni # 32, ambao ni *angelos.*

Kuwa hakika kuendelea kusoma jarida la **The Sacred Name Broadcaster**, kama ninaendelea na somo hili la kuvutia, kushika na kukamata la madarasa manne ya viumbe walioumbwa. Masomo mengi makubwa yatajitokeza kututia moyo kuendelea kwa njia ya wokovu. SNB



# Mnyama Mkali

Geukia kwa Zakaria 11 kwa maandishi ya ya kwanza. ***"Ifungue milango yako EeLebanoni, ili moto uiteketeze mierezi yako. Piga yowe, msonobari, maana mwerezi umeanguka, kwa sababu miti iliyo mizuri imeharibika; pigeni yowe, enyi mialoni ya Bashani, kwa maana msitu wenye nguvu umeangamia. Sauti ya wachungaji, ya uchungu mwingi! Kwa maana utukufu wao umeharibika; Sauti ya ngurumo ya wana-simba! Kwa maana kiburi cha Yordani kimeharibika.***

***"Yahweh, Elohim wangu, alisema hivi, Lilishe kundi la machinjo, ambalo wenye kundi hilo huwachinja, kisha hujiona kwamba hawana hatia; na hao wawauzao husema, Na ahimidiwe Yahweh, kwa maana mimi ni tajiri; na wachungaji wao wenyewe hawana huruma. Maana mimi sitawahurumia tena wenyeji wa nchi hii asema Yahweh; bali, tazama nitawatia, kila mmoja wao, mikononi mwa mwenzake, na mikononi mwa mfalme; nao wataipiga hiyo nchi, wala mimi sitawaokoa mikoni mwao. Basi nikalilisha kundi la machinjo, kweli kondoo waliokuwa wanyonge kabisa. Kisha nikajipatia fimbo mbili; nami nikaiita ya kwanza, Neema, na ya pili nikaiita, Vifungo; nikawakatilia mbali wachungaji watatu katika mwezi mmoja; maana nafsi yangu ilikuwa imechoka kwa ajili yao, na nafsi zao pia walinichukia. Ndipo nikasema, sitawalisheni, afaye na afe, atakayekatiliwa mbali na akatiliwe mbali; nao waliosalia, kila mmoja na ale nyama ya mwili wa mwenziwe. Nikait-***




***waa hiyo fimbo yangu iitwayo Neema, nikaikata vipande viwili, ili nipate kulivunja agano langu nililolifanya na watu wa kabila zote. Nayo ikavunjwa siku ile; na hivyo wale kondoo wanyonge walionisikiliza wakajua ya kuwa neno hili ndilo neno la Yahweh. Nikawaambia, Mkiona vema, nipeni ujira wangu; kama sivyo, msinipe. Basi wakanipimia vipande thelathini vya fedha, kuwa ndio ujira wangu. Kisha Yahweh akaniambia, Mtupie mfinyanzi kima kizuri, hicho nilichotiwa kima na watu hao. Basi nikavitwaa vile vipande thelathini vya fedha, nikamtupia huyo mfinyanzi ndani ya nyumba ya Yahweh. Ndipo nikaikata vipande viwili fimbo yangu ya pili, iitwayo Vifungo, ili nipate kuuvunja udugu uliokuwa kati ya Yuda na Israeli.***

***"Yahweh akaniambia, Jitwalie tena vyombo vya mchungaji mpumbavu. Kwa maana, tazama, mimi nitainua katika nchi hii mchungaji, ambaye hatawaangalia waliopotea, wala hatawatafuta waliotawanyika, wala hatamganga aliyevunjika, wala hatamlisha aliye mzima; bali atakula nyama ya wanono, na kuzirarua-rarua kwato zao. Ole wake mchungaji asiyefaa, aliachaye kundi! Upanga utakuwa juu ya mkono wake, na juu ya jicho lake la kuume; mkono wake utakuwa umekauka kabisa, na jicho lake la kuume litakuwa limepofuka."***

Utafiti wetu wa kitabu cha Ufunuo umekuwa uzoefu wa kuridhisha kwetu. Tumeelewa zaidi ya umuhimu wa makusanyiko saba ya Ufunuo 2 na 3. Jumbe hizi zinakusudiwa kuwatia moyo watu wa Yahweh katika siku hizi za mwisho. Neno la Yahweh limetutia sisi nguvu kiroho, na limetuchukua kwa viwango vipya vya kuelewa kusudi kwa ambalo Mwenye-nguvu Yahweh ametuumba na kutuita sisi. Kama yatazingatiwa, masomo haya yataondoa kwetu wasiwasi kuhusu siku zijazo, kwani tutaweza, kwa maarifa ya mambo yajayo, kuwa na uwezo kujitayarisha wenyewe kwa yaliyo mbele. Katika hili, Mwenye-nguvu Yahweh amebariki watu wake zaidi ya chochote tunachoweza kutaka, ili kwamba tunaweza kufanya kuitwa na kuchaguliwa kwetu hakika.

Mlango wa 11 wa Zakaria unashikilia kwa kiasi fulani utafsiri wa Ufunuo 13. Hapa tunao unabii wa jinsi Mwenye-nguvu Yahweh atawadumisha watu Wake kwa lishe ya elimu. Inaelezea wakati ambapo kila mmoja wetu itabidi kusimama kwa mtihani kibinafsi na kufanya hivyo pekee kwa lishe ya kiroho ambayo kila mmoja wetu amepokea kutoka Juu kupitia Neno la Yahweh kupitia miaka ya kusoma kwetu kwa Maandiko. Kifungu hiki pia kinaelezea jeraha la mauti lililotolewa kwa ambaye anaelezewa kama mchungaji asiyefaa au mchungaji mpumbavu. Bado kifungu hiki kinaelezea nini inafanyika kwa moja ya vichwa vya mnyama wa Ufunuo 13.

Upanga wa Yahweh uko juu ya mchungaji asiyefaa. Mstari wa 17. ***"Ole wake mchungaji asiyefaa, aliachaye kundi! Upanga utakuwa juu ya mkono wake, na ju ya jicho lake la kuume; mkono wake utakuwa umekauka kabisa, na jicho lake la kuume litakuwa limepofuka."*** Mkono uliokauka inamaanisha kwamba hakutakuwa na msaada kwa watu wa Yahweh kutoka kwa huo. Jicho lililopofuka lina maana kwamba mchungaji huyu asiyefaa hana maono kwa watu wa Yahweh. Kwa maneno, mengine, watu wa Yahweh lazima waangalie mbali kutoka kwa huyu kiumbe mpinga Messiah, kwa sababu hawezi wasaidia kwa njia yoyote. Sio Messiah wa Kweli ambaye mkono wake unampa ushindi kwake, ambaye macho yake ni wazi kila wakati na haki ya Yahweh. Na hili ndilo linafanyikia kichwa kilichojeruhiwa hadi kifo, lakini bado anaishi. **Amekufa kiroho**, lakini, bado, anaishi kufanya uharibifu kwa watu wa Yahweh. Hiki ni kifungu kikubwa (Zakaria 11).

Kama tunarudi nyuma kwa Ufunuo 13, tunataka kurejelea mambo fulani. Kunao mfanano kati ya wanyama wawili ambao wanaelezewa katika Ufunuo 13.


Kwanza, wanakuja kutoka mahali tofauti, na bado sawa. Wanakuja kutoka duniani, sayari ya dunia. Mmoja anakuja kutoka baharini; mwingine anakuja kutoka katika nchi. Ufunuo 13:1: ***"Naye akasimama juu ya mchanga wa bahari, na nikaona mnyama akitoka katika bahari, mwenye pembe kumi,na vichwa saba, na juu ya pembe zake ana vilemba kumi, na juu ya vichwa vyake majina ya makufuru."*** Mstari wa 11 ***"Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi; naye alikuwa na pembe mbili mfano wa Mwana-Kondoo, akanena kama joka.***" Ulimwengu unastaajabia mnyama, kustaajabia katika mshangao.

Mstari wa 3: ***"Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti, na pigo lake la mauti likapona. Dunia yote ikastaajabu mnyama yule...."*** Mstari 12: ***"Naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake. Naye aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama wa kwanza, ambaye jeraha lake la mauti lilipona."*** Angalia, dunia yote itamwabudu mnyama wa kwanza na wa pili.

Mstari wa 4: ***"Wakamsujudia yule joka kwa sababu alimpa huyo mnyama uwezo wake; nao wakamsujudia yule mnyama, wakisema, Ni nani afananaye na mnyama huyu? Tena ni nani awezaye kufanya vita naye?"*** Na kisha mstari wa 8: ***"Na watu wote wakaao juu ya nchi watamsujudu, kila ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa msingi wa dunia."*** Na, kisha, mstari wa 12: ***"Naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake. Naye aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama wa kwanza*** [je, unaona mfanano?], ***ambaye jeraha lake la mauti lilipona."*** Dunia yote itawaabudu wanyama hawa wawili. Uabudu wa Shetani unasimama nyuma ya ibada ya mnyama.

Na wakamwabudu Joka, katika mstari wa 4, ambaye tunapata katika Ufunuo 12:9 ni Ibilisi (Shetani). ***"Wakamsujudia yule joka kwa sababu alimpa huyo mnyama uwezo wake; nao wakamsujudia yule mnyama, wakisema, ni nani afananaye na mnyama huyu? Tena ni nani awezaye kufanya vita naye?"*** (Ufunuo 13:4).

Tena, katika Ufunuo 13:11-12: ***"Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi; naye alikuwa na pembe mbili mfano wa***



***Mwana-kondoo, akanena kama joka*** [kama Ibilisi, Shetani]. ***Naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake. Naye aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama wa kwanza....”*** Na tumesoma tu ni nani yuko nyuma ya mnyama wa kwanza na huyo ni Shetani Ibilisi. Vitu hivi kweli ni mafundisho yenye nguvu. Wanyama hawa wote wanao mdomo.

Katika Ufunuo 13:5: ***“Naye akapewa kinywa cha kunena maneno makuu, ya makufuru....”*** Na mstari wa 11: ***“Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi; naye alikuwa na pembe mbili mfano wa Mwana-kondoo, akanena kama joka.” Na mstari wa 15: “Akapewa kutia pumzi katika ile sanamu, hata kwa sanamu ya mnyama, ili kwamba sanamu ya mnyama inene, na kuwafanya hao wote wasioisujudu sanamu ya mnyama wauawe.”*** Mdomo ni wa nini? Mdomo unakusudiwa kukufuru Yahweh na watu Wake.

Mstari wa 5: ***“Naye akapewa kinywa cha kunena maneno makuu, ya makufuru....”*** Mstari wa sita: ***“Akafunua kinywa chake amtukane Yahweh, na kulitukana jina lake, na maskani yake, nao wakaao mbinguni.”*** Na kisha mstari wa 13: ***“Naye afanya ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu. Naye akawakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya mbele ya huyo mnyama; akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi.”*** Utaona kwamba mnyama wa pili ndiye mponyaji wa jeraha la mauti la myama wa kwanza. Unapogundua katika

***Kama yatazingatiwa, masomo haya yataondoa kwetu wasiwasi kuhusu siku zijazo, kwani tutaweza, kwa maarifa ya mambo yajayo, kuwa na uwezo kujitayarisha wenyewe kwa yaliyo mbele. Katika hili, Mwenyenguvu Yahweh amebariki watu wake zaidi ya chochote tunachoweza kutaka, ili kwamba tunaweza kufanya kuitwa na kuchaguliwa kwetu hakika.***

mstari wa tatu: ***“Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti....”*** Na kisha inasema anaifanya dunia na wao wanaokaa ndani yake kumwabudu mnyama wa kwanza ambaye jeraha la mauti liliponywa.

Kwa muda mfupi tu basi tugeukie kwa Ufunuo 17. Tunasoma hapo katika mstari wa 11: ***“Na yule mnyama aliyekuwako naye hayuko, yeye ndiye wa nane, naye ni mmoja wa wale saba, naye aenenda kwenye uharibifu.”*** Vizuri, kunayo mambo fulani makubwa unapoanza kuweka Maandishi haya upande kwa upande. Wote wanafanya mamlaka au uongozi, juu ya ulimwengu. Kwa njia fulani watadhibiti dunia yote. Mstari wa 7: ***“Tena akapewa kufanya vita na watakatifu na kuwashinda, akapewa uwezo juu ya kila kabila na jamaa na lugha na taifa. Na watu wote wakaao juu ya nchi wakamsujudu.”*** Na kisha mstari wa 16: ***“Naye akawafanya wote, wadogo kwa wakubwa*** [vyema, je, hilo halijumuishi kila mtu? Wadogo na wakubwa, wadogo na wakuu, na walio huru] ***na matajiri kwa maskini*** [hilo linajumuisha kila mtu] ***na walio huru kwa watumwa*** [hilo linajumuisha kila mtu- walio watumwa na walio huru, kila mtu duniani amejumuishwa katika makundi hayo matatu], ***watiwe chapa katika mkono wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao; tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile.”*** Wanyama wote wanao udhibiti juu ya maisha, haswa maisha ya watakatifu. Mstari wa 10 ***“Kama mtu ni wa kuchukua mateka, atachukuliwa mateka. Mtu akiua kwa upanga, atauawa kwa upanga. Hapa ndipo penye subira na imani ya watakatifu.”***

Mstari wa 15: ***“Akapewa kutia pumzi katika ile sanamu ya mnyama, hata kwa sanamu ya mnyama, ili kwamba sanamu ya mnyama inene, na kuwafanya hao wote wasioisujudu sanamu ya mnyama wauawe.***” Wanyama watadhibiti biashara.

Ufunuo 14:13: ***“Nikasikia***

***sauti kutoka mbinguni ikisema, andika, Heri wafu wafao katika Yahshua tangu sasa. Naam, asema Roho, wapate kupumzika baada ya taabu zao; kwa kuwa matendo yao yafuatana nao,"*** Kupumzika kutoka kwa kazi zao.

Ufunuo 13:17 ***"Tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake."***

Basi tusisahau, mnyama wa pili anatumia nguvu yote ya mnyama wa kwanza, mstari wa 12, ***"Naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake."*** Na ni wa kishetani. Mstari wa 2: ***"Yule joka akampa nguvu zake na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi."*** Unaelewa, mnyama wa pili anatumia nguvu yote ya kishetani ambaye anasimama nyuma ya mnyama wa kwanza. Hilo linamaana ya kifo kwa wote ambao watapinga, kwa wote ambao hawatatumikia wanyama hawa.

Mstari wa 4: ***"Wakamsujudia yule joka kwa sababu alimpa huyo mnyama uwezo wake; nao wakamsujudia yule mnyama, wakisema, ni nani afananaye na mnyama huyu? Tena ni nani awezaye kufanya vita naye?"*** Mstari wa 7: ***"Tena akapewa kufanya vita na watakatifu na kuwashinda, akapewa uwezo juu ya kila kabila, na jamaa, na lugha, na taifa."*** Hivyo, kama atawashinda watakatifu, pia ataweza kumdhibiti kila mtu mwingine.

Mstari wa 10: ***"Kama mtu ni wa kuchukua mateka, atachukuliwa mateka. Mtu akiua kwa upanga, atauawa kwa upanga."*** Na mstari wa 15 tena: "Akapewa kutia pumzi katika ile sanamu ya mnyama, hata kwa sanamu ya mnyama, ili kwamba sanamu ya mnyama inene, na kuwafanya hao wote wasioisujudu sanamu ya mnyama wauawe."

Kifo kitatolewa kwa wote ambao hawatawatumikia wanyama hawa. Kichwa cha nakala hii ni Mnyama Mkali. Waandishi kama vile Elie Wiesel, na wachanganuzi wengine, walitoa maoni kuhusu utawala wa Nazi wa Vita vya Pili vya Dunia, kwamba ulikuwa mnyama anayemeza roho, mnyama ambaye alimeza Wayahudi 6,000,000, mnyama ambaye alimeza watu wengine milioni 6 ambao waliteswa, mnyama ambaye alimeza askari waliotumiwa kupigana kwenye uwanja wa Vita vya Pili vya Dunia. Mnyama huyu ni mgani?

Kwa muda mfupi, ruhusu tuelewe zaidi kuhusu neno mnyama. Mhubiri 3:18. ***"Nikisema moyoni mwangu, ni kwa sababu ya wanadamu, ili Elohim awajaribu, nao waone ya kuwa wao wenyewe wafanana na wanyama."*** Unaona, kaka na dada, Yahweh Elohim anawajaribu wanadamu kwa sababu kwa kweli ni kama wanyama. Wanafikiria karibu tu kama wanyama. HAWANA UPENDO MOYONI MWAO ISIPOKUWA KWAO WENYEWE. Hawana mazingatio kwa wengine. Kwa hivyo, ni muhimu kwamba lazima wabadilishwe, mioyo yao lazima ibadilike. Angalia tena, ***"Nikisema moyoni mwangu, ni kwa sababu ya wanadamu, ili Elohim awajaribu…."*** Yahweh lazima aone nini iko moyoni mwao. Yahweh ametoa na kutawaza juu ya binadamu wanaotaka kuupokea. Roho Mtakatifu anazaa matunda mema, matunda la Roho Mtakatifu ni hilo la upendo na furaha na amani. Lakini, kusikitisha, mtazamo wa watu ni kama tu Paulo anavyowaelezea katika 2 Timotheo 3, ambapo hatimaye anasema, ***"Lakini watu wabaya na wadanganyaji wataendelea, na kuzidi kuwa waovu, wakidanganyana na kudanganyika."*** Tambua nini walio.HAWANA mapenzi ya asili; hawana kiasi; wao ni WAKALI, wakiwa na aina ya haki, lakini wameikataa nguvu yake.

Basi tusisahau Zaburi 49:12, ambayo inatuambia, ***"Lakini mwanadamu hadumu katika heshima, bali amefanana na wanyama wapoteao."*** Na hiyo ni nini? Vizuri, hao bila shaka ni watu waovu wanaoishi duniani. Kuteremka chini kwa mstari wa 20, ***"Mwanadamu mwenye heshima, iwapo hana akili, amefanana na wanyama wapoteao."*** Wale ambao hawataki kupata maarifa ni kama wanyama wanaoangamia. Si ajabu nabii Isaya anaweza kusema katika mlango wa 18, kuanzia katika mstari wa 4 ***"Maana Yahweh ameniambia hivi, Mimi nitatulia, na kuangalia katika makazi yangu, kama wakati wa mwangaza mweupe wa jua kali,mfano wa wingu la umande katika hari ya mavuno."*** Mwanzo wa kifungu, mistari ya kwanza 3, inaelezea Marekani kabisa tangu mwanzo. Ha hiyo anasema, ***"Mimi nitatulia, na kuangalia katika makazi yangu[nitakuwa mvumilivu tu], kama wakati wa mwangaza mweupe wa jua kali*** [wakati kila kitu kimetulia, huyo atakuwa mimi], ***mfano wa wingu la umande katika hari ya mavuno."*** Huyu atakuwa mimi aliyetulia na katika amani na mambo yote yametulia- hakuna upepo unaovuma. Nitaona nini itafanyika.***"Maana kabla ya mavuno, maua yaangukapo, na maua yakawa zabibu zianzazo kuiva, ndio atakapoyakata matawi kwa miundu, na kuviondoa vitawi vilivyopanuka na kuvikata. Wote pamoja wataachiwa ndege wakali wa***




University of Texas Tower

***milimani, na hayawani wa nchi."*** Unaelezewa wakati Yahweh anatazama, wanyama wa dunia watawajia watu hawa (taifa hili), "***na hayawani wote wa nchi watakaa juu yao wakati wa baridi. Wakati huo Yahweh wa majeshi ataletewa hedaya na watu warefu, laini; watu watishao tangu mwanzo wao hata sasa; taifa la wenye nguvu wakanyangao watu, ambao mito inagawanya nchi yao*** [Neno kugawanya linamaanisha kugawa katika robo]; ***mpaka mahali pa jina la Yahweh wa majeshi, mlima Sayuni."*** Hilo ni kutoka kwa watu ambao wanayo mioyo mizuri; watu walioongoka ambao watakuwa wakileta sadaka hiyo.

Lakini nini itafanyika kwa wengine? Hatimaye, Yahweh atawaondoa. Isaya 30:6: ***"Ufunuo juu ya hayawani wa Kusini*** [kunao hata unabii, unaoweza kusema ni wa Misri na mataifa ya Afrika]. ***Katikati ya nchi ya taabu na dhiki, ambayo hutoka huko simba jike na simba, nyoka na joka la moto arukaye, Huchukua mali zao mabegani mwa punda wachanga, na hazina zao juu ya nundu za ngamia, waende kwa watu ambao hawatawafaa kitu. Kwa maana Misri huwasaidia bure, bila faida; kwa hiyo nimemwita, Rahabu aketiye kimya."*** Watu hawa ni kina nani? Watu ambao wanapaswa kujua vizuri. WAPASWA KUWA WAKIMTAFUTA YAHWEH. Lakini wanafanya nini sasa? ***"Haya enenda sasa, andika neno hili katika kibao mbele ya macho yao, lichore katika kitabu ili liwe kwa ajili ya majira yatakayokuja, kwa ushuhuda hata milele. Kwa kuwa ni watu waasi, watoto wanaodanganya, watoto ambao hawatasikia sheria ya Yahweh...."*** Hao ni watu ambao wanaenda na kujaribu kununua fadhila kutoka kwa mataifa, na hazina za mataifa haya zinatupwa kwa watu ambao kamwe hawatafaidika. ***"Wawaambiao waonaji, Msione; na manabii, Msitoe unabii wa mambo ya haki, tuambieni maneno laini, hubirini maneno yadanganyayo; tokeni katika njia, geukeni mtoke katika mapito; mkomesheni Mtakatifu wa Israeli mbele yetu. Basi kwa ajili ya hayo, kwa sababu mwalidharau neno hili, na kutumaini jeuri na ukaidi, na kuyategemea hayo; basi uovu huo utakuwa kwenu kama mahali palipobomoka."***

Nilijumuisha Danieli 7:17 awali, lakini tunataka kukumbushwa kuihusu, kwa sababu inatuelezea nini mnyama anamaanisha. Danieli 7:17: ***"Wanyama hao wakubwa walio wanne ni wafalme wanne watakaotokea duniani."*** Hivyo hatuna haja kukisia mnyama ni nani, au mnyama ni nini. Ni mfalme, au falme au himaya. Unapoangalia kwa kifungu katika Danieli mlango wa 7, unakilinganisha kwa Danieli mlango wa 2 na vifungu vingine. Kisha unaweza kusema aha,



2025 New Orleans Terror Attack

inazungumzia kuhusu himaya zinazotawala ulimwengu ambazo ni Babeli, Media, Uajemi, Ugiriki, na Rumi. Kutambua mnyama, mtu pia anawezatumia Mika 5:8. ***"Na hayo mabaki ya Yakobo yatakuwa kati ya mataifa, kati ya kabila nyingi, mfano wa simba kati ya wanyama wa msituni, kama mwana-simba kati ya makundi ya kondoo...."*** Hivyo hapa mnyama miongoni mwa wanyama, Yuda miongoni mwa mataifa ya ulimwengu, mabaki ya Yakobo, sio tu Yuda, lakini mabaki ya Yakobo, ambayo ni Waisraeli.


Katika 2 Petro 2:12. ***"Lakini hao kama wanyama wasio na akili,ambao walizaliwa kama wanyama tu wa kukamatwa na kuangamizwa."*** Katika New Zealand, 1990, mtu alichukua bunduki ya kushambulia na kuanza kuwapig risasi watu, na wakaleta kikosi cha kupambana na ugaidi na kumpiga risasi. Walitoa sababu kwamba tayari alikuwa ameua watu 13, na hakuwa karibu kuacha. Ilibidi wamsimamishe kama mbwa mwendawazimu katika mtaa. Hivyo ndivyo watu hufanya wakati hawana Roho Mtakatifu wa Yahweh. Wakidhibitiwa na Shetani, wanajaribu kuharibu, wanajaribu kuua, na hawajali. Hawajali kuhusu wao wenyewe. Wao ni kama wanyama ambao ni wa kuchukuliwa na kuangamizwa kabla ya kuangamiza watu wengi zaidi. Ni mara ngapi tunaiona hapa katika Marekani? Tunaisikia kwenye habari mpya. Mtu fulani anachukua bunduki, au kisu au kugongesha gari kwenye umati wa watu. Mtu fulani alipiga risasi karibu watu 50 kutoka mnara wa saa katika Chuo Kikuu cha Texas. Hatimaye, iliwabidi kufanya jambo sawa kwake.Hawakuwa wachukue mbwa mwendawazimu huyo akiwa hai.Kisha wakampiga risasi kwa sababu alikuwa kama mnyama. Hilo ndilo Petro anasema.Hili ndilo Biblia nzima inatuambia. Mtu, bila Roho Mtakatifu, anaelekea kutoka mbaya hadi mbaya zaidi. Hii ndiyo sifa ya mataifa, viongozi wa mataifa ni kama Nimrodi. Wanaelekea kutoka mbaya hadi mbaya zaidi.

Yuda mstari wa 10: ***"Lakini watu hawa huyatukana mambo wasiyoyajua, na mambo wayatambuayo kwa asili, wajiharibu kwayo kama wanyama wasio na akili."*** Je, hilo sivyo watu wa kidunia wanafanya? Wanakemea kwa vitu ambavyo hawajui, wasioelewa, na bado, wanayo maoni-wataalamu wa papo kwa hapo- na wanayo maoni ambayo yatawaondoa kutoka kwa Yahweh. Kama tu wanyama wasio na akili, kukimbia, kukimbia, kukimbia, wanapofunguliwa, na huwezi kuwasimamisha. Wanakimbia mbali,na milele wanapotea. Watakimbia kwenye mwamba na kujiua wenyewe. Hilo ndilo hasa nini Yuda anajaribu kutuonyesha. Binadamu bila Roho Mtakatifu wa Yahweh, bila Agano Lake kumzuia, kumwekea vikwazo, kuashiria njia sahihi ni kama wanyama. Ni kama wanyama ambao wanaangamia. SNB




**Juzuu ya pili ya msururu wa Commentary on the Book of Revelation sasa inapatikana kwa usambazaji. Unaweza andika kwa Assemblies of Yahweh PO Box C. Bethel PA 19507, au upige nambari ya ofisi kuu (717) 933-4518, kupokea ujumbe zaidi jinsi unavyoweza kununua kopi ya kitabu hiki.**

**Assemblies of Yahweh**
**PO Box C • Bethel, PA 19507**
**(717) 933-4518**
**www.assembliesofyahweh.com**



# THE LAW OF YAHWEH

## Amri ya Kumi

# Usitamani

Na Mzee Jacob O. Meyer

***"Ikawa baada ya hayo, Nabothi Myezreeli alikuwa na shamba la mizabibu katika Yezreeli, karibu na ikulu ya Mfalme Ahabu wa Samaria. Ahabu akasema na Nabothi, akamwambia, Nipe shamba lako la mizabibu nilifanye shamba la mboga, maana ni karibu na nyumba yangu; nami nitakupa badala yake shamba la mizabibu lililo zuri zaidi; au ukipenda, nitakupa, fedha sawasawa na thamani yake. Nabothi akamwambia Ahabu, Yahweh apishe mbali, nikupe wewe urithi wa baba zangu. Basi Ahabu akaenda nyumbani kwake, ana moyo mzito, tena amekasirika, kwa sababu ya neno lile aliloambiwa na Nabothi Myezreeeli, akisema, sitakupa urithi wa baba zangu. Akajilaza kitandani pake, akageuza uso wake, akakataa kula.***

***"Lakini Yezebeli mkewe, akamwendea akamwabia, Kwa nini roho yako ina huzuni hata usile chakula? Akamwambia, Kwa sababu nimesema na Nabothi Myezreeli nikam-***

***wambia, Unipe shamba lako la mizabibu kwa fedha, au, ukipenda, nitakupa shamba la mizabibu lingine badala yake. Akajibu, sitakupa shamba langu la mizabibu. Yezebeli mkewe akamwambia, Je! Sasa wewe unaumiliki ufalme wa Israeli? Ondoka, ule chakula, moyo wako ufurahi; mimi nitakupa shamba la mizabibu la Nabothi Myezreeli. Basi akaandika nyaraka kwa jina la Ahabu, akatia muhuri yake, akazipeleka zile nyaraka kwa wazee, na kwa watu wenye nguvu waliokuwa katika mji wake, waliokaa pamoja na Nabothi. Akaandika katika zile nyaraka, akasema, pigeni mbiu ya watu kufunga mkamweke Nabothi juu mbele ya watu, mkainue watu wawili, watu wasiofaa, ili wamshitaki, na kumshuhudia, kunena, umemtukana Elohim na mfalme. Kisha mchukueni nje, mkampige kwa mawe, ili afe.***

***"Wale wazee wa mji wake, na walio wenye nguvu waliokaa mjini mwake, wakafanya kama Yezebeli alivyowaagiza, kama ilivyoandikwa katika nyaraka alizowapelekea. Wakapiga mbiu ya watu kufunga, wakamweka Nabothi juu mbele ya watu. Na hao watu wawili, watu wasiofaa, wakaingia, wakaketi mbele yake; wale watu wasiofaaa wakamshuhudia Nabothi mbele ya watu, wakasema, Nabothi amemtukana Elohim na mfalme. Ndipo wakamchukua nje ya mji, wakampiga kwa mawe hata akafa. Wakampelekea Yezebeli habari, wakasema, Nabothi amepigwa kwa mawe, amekufa. Ikawa Yezebeli aliposikia ya kwamba Nabothi amepigwa kwa mawe na kufa, Yezebeli akamwambia Ahabu, Inuka ulitamalaki shamba la mizabibu la Nabothi Myezreeli, alilokataa kukupa kwa fedha, maana Nabothi hako hai, lakini amekufa. Ikawa Ahabu aliposikia ya kwamba Nabothi amekufa, akaondoka, alitelemkie shamba la mizabibu la Nabothi Myezreeli, ili alitamalaki.***

***"Neno la Yahweh likamjia Eliyah Mtishbi, kusema, Ondoka, ushuke, ukutane na Ahabu mfalme wa Israeli, akaaye katika Samaria, yuko katika shamba la mizabibu la Nabothi, ndiko alikoshuka ili alitamalaki. Ukamwambie, ukisema, Yahweh asema hivi, Je! Umeua, ukatamalaki? Nawe utamwambia kusema, Yahweh asema hivi, Mahali pale mbwa walipoiramba damu ya Nabothi, mbwa watairamba na damu yako, naam, damu yako. Ahabu akamwambia Eliyah, Je! Umenipata, ewe adui yangu?Akamwambia, nimekupata, kwa sababu umejiuza utende yaliyo mabaya machoni pa Yahweh."*** (1 Wafalme 21:1-20).

Mada ya somo letu leo katika Neno la Yahweh litakuwa Amri ya Kumi, inayopatikana katika Kutoka 20:17. ***"Usiitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako; wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala chochote alicho nacho jirani yako."*** Angalia pia Kumbukumbu la Torati 5:21.

Mtu wakati fulani anajiuliza kwa nini amri hii iliwekwa mwishoni mwa Sheria ya Yahweh, wakati inapoonekana kwamba zingine zote za ukiukaji wa amri (kwa kanuni) zinakalia kwa msingi wa ya kumi. Mwenye-nguvu Yahweh alipowaita watu Wake Israeli, aliwapa sheria ambazo ni za kuishi, sheria ambazo zingewaletea wao furaha pekee kama zingetiiwa kwa dhati yote. Yahweh aliwasilisha amri hizi 10 kama moyo, msingi wa Amri Zake.

Amri hii kweli ndiyo inayopiga kwa nguvu kwa mzizi hasa wa kuharibika kwa maadili ambao tunatambua kote kando yetu leo katika kupenda mali, tamaa, kutafuta raha, jamii ya kidunia. Kamusi inafafanua neno kutamani kama *kujiingiza katika tamaa iliyokithiri, au haramu, hamu ya kupita kiasi kwa kupata na kumiliki.* Neno la Kiebrania linaloonekana katika maandiko ya kibiblia ni c*hamad* (#2530 katika **Strong's Concordance**). Linamaanisha *kufurahiya, kutamani, au kutamani yanayopendeza akilini.*

Yahweh Mwenye-nguvu, Muumbaji na Mfadhili wa ulimwengu wote, hataki chochote zaidi kutoka kwa watu Wake kuliko utiifu, ibada safi na sifa. Tunapata kwamba mara mingi sana, watu wanakataa tu kukubali kwamba wanaweza kuwa na makosa kuhusu chochote. Watu ambao hawajaongoka wanataka tu kujiwekea kiwango cha kibinafsi cha maadili ambacho wanaweza kutii bila usumbufu.Hawatamruhusu yeyote sio hata Yahweh Mwenye-nguvu, kuwaambia wao nini kiwango kinapaswa kuwa. Hawatavumilia hata kidogo uongozi wowote juu yao. Hata hivyo, unabii wa Biblia unatuarifu kwamba watakuwa na kiongozi kwa njia yoyote katika siku zijazo wakati Mwokozi, Yahshua aliye Messiah ataanzisha Ufalme wa Yahweh duniani- au wataangamia milele kama hawatajiwasilisha kwa hiari kwa uongozi wa haki.

Wakati Yahweh aliwaita watu Wake Israeli kutoka Misri, aliwaamuru wao kuamini pekee katika Jina Lake, kumwabudu Yeye—katika roho na katika kweli, na wasiruhusu sanaa za kidini au

picha. Yahweh aliwaambia watu Wake kumwabudu Yeye pekee katika siku maalum ambayo aliweka kando na kuitakasa kwa kusudi hilo. Walakini, chini kupitia historia ya Israeli, watu hawa wenye shingo ngumu hawangemsikiliza; kinyume chake, walitamani ibada ya kidini ya majirani wao wa mataifa. Kwa fursa ya kwanza, Israeli haraka aliasi kukumbatia uabudu wa uongo wa upagani. "Tunataka kuwa kama majirani yetu," walisisitiza. "Tunataka kuunganishwa kwenye umati na jamii.Tunataka kuwa waliotoshea vizuri. Tunataka kutoshea kwenye jamii ya kidunia, kutekeleza kuvumiliana na usawazishaji wa kidini."

Geukia kwa kitabu cha nabii Ezekieli, mlango wa 20, mstari wa 32. ***"Na hayo yote yaingiayo katika nia zenu hayatakuwa kamwe; kwa kuwa mnasema, sisi tutakuwa sawasawa na mataifa, sawasawa na jamaa za nchi nyingine, kutumikia miti na mawe."***

Tambua kwamba Israeli alitamani kwa hamu sana ibada ya sanamu ya elohim wa upagani (wenye-nguvu). Walitaka kuunganishwa kwenye mfumo huu wa kidunia, kuonekana kama familia za upagani, au nchi za mataifa ya ulimwengu.

Katika mistari kadhaa inayofuata Yahweh anatangaza kwamba atalituma taifa nzima la Israeli tena kwenye hali ya nyikani na kuwasihi huko. Kwa wazi anakusudia kuwatenganisha kutoka kwa mataifa na kusahihisha kufikiria kwao kwenye makosa. Atawaondoa waasi, na kuwaleta kwenye kifungo cha agano, ambayo inawakilisha utiifu madhubuti kwa amri 10 na Sheria za maadili zinazohusiana kama zilivyowekwa katika Torati (sheria) ya Yahweh.

Sasa gundua mstari wa 39 wa Ezekieli, mlango wa 20. ***"Na katika habari zenu, enyi nyumba ya Israeli, Mwenye-Enzi Yahweh asema hivi, enendeni, mkazitumikie sanamu zenu kila mmoja wenu, wakati wa baadaye pia kama hamtaki kunisikiliza; lakini jina langu takatifu hamtalitia unajisi tena, kwa matoleo yenu, na kwa sanamu zenu."*** "Endelea," Yahweh anatangaza, ***"fanyeni uzinzi wa kiroho, lakini msihusishe Jina Langu na chukizo hizi. Jina langu kuu kamwe halitaunganishwa na ibada ya upagani, au uabudu wa sanamu."***

Leo, tunaweza kutambua nini imefanyika kwa ibada safi ya Yahweh. Jamii mingi zinakataa hata kutambua Jina Lake kuu. Wanajiita *mataifa* ambalo katika Maandiko linaashiria *mpagani asiyeamini wa asili ya kikabila.* Wanakataa kutambua kitu kama Agano na Mwenye-nguvu-Agano la utiifu kwa Sheria (torati) Yake ambayo inaonyesha kwa ulimwengu, Aliye na Nguvu mgani watamtumikia. Wanafikiria kwamba kwa aina fulani ya kutoa kwa hisia ya MOYO wako kwa Mwokozi na MKONO wako kwa k-nisa, unaweza kisha kuendelea na kuishi kama tu ulivyofanya kila mara. Wanadai kwamba dhambi zako zitasamehewa na utaenda mbinguni utakapokufa- dhana ambayo si ya kimaandiko kabisa na kwa kweli ni fundisho la uongo, lakini watu dhahiri wanafikiria kwamba dini inavutia wengi zaidi katika njia hii. "Mradi tu sichezi ngoma, kulewa, kucheza kadi (kupita kiasi) unaweza kukiuka yoyote ya amri zingine," wanafunza wengi wa watumishi. Hadi kwa siku hii, wanaendelea kuazima kutoka kwa dini za kale za Misri, Babeli, na Mwashuri nk., kwa sababu mafundisho ya dini hizo ni maarufu zaidi. Pengine mafundisho yalisikika mazuri zaidi na ya kupendeza zaidi kwa masikio, lakini Yahweh anatangaza kuwa hazitakuletea wokovu wa milele.

Sio tu watu wametamani mila za kigeni za dini , na wameiin-



giza mafundisho haya ya uongo kama mbadilisho kwa ukweli wa Biblia, lakini katika dini yao mpya, ghafla wamegeukia kwa kupenda mali ambalo bila shaka wametamani mali ya majirani zao. Umewahi kusikia usemi "watu wakishindana kuwa sawa na akina Joneses?" Hapa ni mfano: jirani yangu nyumba kadhaa karibu nami amepata tu gari ndogo mpya, hivyo lazima nikimbie sasa na ninunue Cadillac mpya! Hata kama siwezi kumudu baiskeli, itabidi tu niingie ndani kwenye deni nikae mbele ya jirani yangu aliye karibu, kwa hivyo, familia yangu itateseka, lakini hakika tumeenda hatua juu ya Joneses, jirani yangu wa karibu.

Leo, jarida kubwa za habari zinachapisha hadithi baada ya hadithi, wakiripoti kuwa deni la kibinafsi la Marekani linaendelea kupanda zaidi, deni ambalo sasa linafika kwa trilioni mingi za dola, deni ambalo liko karibu kuzizidi famiilia mingi na kuzisukuma kwenye kufilisika kwa kibinafsi. Hata katika serikali ya kitaifa, Mbunge linaonekana lisilo na wasiwasi kuhusu shida la kifedha linaloishika nchi hii. Falsafa ya "kuwa nayo kabla ya kupata," imeelekeza familia nyingi kukopa kiasi kikubwa cha pesa kwa riba kubwa mno. Deni ya kitaifa pia sasa imepanda kwa zaidi ya dola trilioni 15, takwimu ambayo akili ya binadamu haiwezi kuanza kuelewa.

Serikali zinatamani rasilimali za madini ya nchi jirani, kama vile bandari au njia za bahari, kujitumbukiza wenyewe kwenye vita ambavyo mamilioni ya maisha yasiyo na hatia yanaangamizwa, wakati wanakabiliana na mashine hizi zenye nguvu za kijeshi za nyakati za kisasa. Ni lini binadamu atajifunza kutosheka na sehemu yake? Watu pengine watajibu, "kamwe la."Lakini ningejibu, "binadamu ataridhika wakati ufalme wa mbinguni utakaribisha zama zilizotabiriwa za haki."

Katika kifungu cha kimaandiko tulichokisoma mwanzoni mwa nakala hii, utagundua dalili ya dhambi hii hasidi ya kutamani. Ahabu, Mfalme wa Nyumba ya Israeli (kabila 10 za kaskazini za Israeli) alikuwa aliyevutiwa sana kwa shamba la mizabibu lililomilikiwa na mtu mwingine- Nabothi. Lilikuwa karibu na ikulu yake na rahisi sana kwake kutumia kama chanzo cha mboga freshi kwa meza yake. Alimuuliza Nabothi amuuzie sehemu hii ya ardhi, au kuifanyia biashara kwa shamba iliyo mbali kwenye nchi. Walakini, Nabothi alinuia kutii Sheria ya Yahweh, ambayo inasema kwamba mtu ataridhi ardhi ya babake na kamwe hataiuza nje ya jina la familia. Yahweh alikuwa ametoa ardhi kwa makabila ya Israeli kwa kura. Hata ilipouzwa, urithi wa familia bado ungerudi kwa mmiliki asili katika mwaka wa Yubile; kwa hivyo, katika athari, ardhi ilikuwa tu iliyokondishwa kwa wakati chini ya miaka 50. Angalia Walawi 25:23-28. Wakati Nabothi alikataa kuuza shamba la mizabibu yake, Mfalme Ahabu kweli alikuwa mgonjwa kimwili kutoka kwa tamaa hii ya kupita kiasi na kutamani, kwamba hangepata njia ya kuipunguza.Kukataliwa alikohisi Ahabu pia kunaonekana kumuathiri kisaikolojia.




*Overlooking site of Naboth's vineyard, Jezreel Valley, Israel*

Sasa anaingia Yezebeli, bibi Mkanani wa Ahabu. "Kwa nini u mgonjwa?"Anauliza.Wewe ndiwe mfalme.Unaweza fanya CHOCHOTE moyo wako unachotamani katika ufalme. Niachie tu kila kitu na karibuni utapata shamba la mizabibu la Nabothi. Hivi ndivyo tutafanya. TUTAMSHTAKI KWA UONGO (KUMPANGIA) mtu huyu asiyebadilika na kumfanya auawe. Atakapoaga, unaweza kuchukua mali, na hutakuwa na kuingiliwa kwa aina yoyote kutoka kwa mtu wa kawaida."

Hilo ndilo hasa walilofanya! Serikali inaidhinisha uongo. Yezebeli aliandika barua kwa sahihi ya Mfalme Ahabu na muhuri wa serikali. Nabothi aliletwa kwa korti, akashtakiwa na mashahidi wa uongo kwa kufuru, na kuhukumiwa na hawa mashahidi wa uongo. Hukumu, kulingana na sheria ya kimaandiko ilikuwa kifo ambacho kilifanyika mara moja kama sheria inavyoamuru pia. Angalia Walawi 24:13-16. Hata hivyo Mwenye-nguvu Yahweh anaona yote na anajua yote, na anadumisha udhibiti juu ya uumbaji Wake. Alimtuma EliYah nabii kumkabili Mfalme Ahabu na ujumbe huu, ***"Ukamwambie, ukisema, Yahweh asema hivi, Je! Umeua, ukatamalaki? Nawe utamwam-***

***bia kusema, Yahweh asema hivi, mahali pale mbwa walipoiramba damu ya Nabothi, mbwa watairamba na damu yako, naam, damu yako."*** (1 Wafalme 21:19). Na utimilifu huu wa baadae ulifanyika sawasawa kama Yahweh alivyomwambia Eliyah, nabii. Wakati Mfalme Ahabu aliuawa katika vita na Siria, watumishi wake waliosha damu yake kutoka kwa gari ya vita katika bwawa la Yezereli, 1 Wafalme 22:33-40.




Katika Waefeso mlango wa 5, dhambi hii ya kutamani imerekodiwa na dhambi zilizoenea za binadamu. ***"Maana neno hili mnalijua hakika, ya kwamba hakuna mwasherati wala mchafu WALA MWENYE TAMAA, NDIYE MWABUDU WA SANAMU, aliye na urithi katika ufalme wa Messiah na Yahweh."*** Maneno wazi kabisa, haukubaliani? Kutamani pia ni kisawe na uabudu wa sanamu, anatangaza Paulo. Inawezekana kuwa kwamba una hatia ya uabudu wa sanamu kwa sababu unatamani kitu ambacho sio chako kuwa nacho?

Dhambi ya kutamani ni moja ambayo ni ngumu kutambua katika maisha ya mtu kwa sababu **imefichwa kwa undani moyoni.** Watu wanaweza kufikiria kwa siri kwa muda mrefu kuhusu ngono haramu, kuhusu kumiliki gari mpya, au kupata mali wasiyo mudu kununua. Watu fulani hufikiria kwa siri kuhusu kuiba banki, au kuua adui wanaomchukia. Hata marafiki wao wa karibu hawawezi kutambua kina cha dhambi inayokaaa imefichwa moyoni mwa mtu asioongoka. Hata hivyo, Yahweh anajua! (Angalia Yeremia 17:9-10.)

Yahweh anatupa fursa kudhibiti mienendo yetu. Lazima tusukume mawazo mabaya ya kutamani nje kabisa ya fikra zetu na kufanya hivyo mara moja Shetani anapoyaingiza. Kama mawazo yataruhusiwa kudhoofika hapo, kweli yatapanda kwa uso siku fulani kuzaa matunda mabaya. Yahshua aliye messiah anafunua jinsi hilo litafanyika. ***"Akasema, kimtokacho mtu ndicho kimtiacho unajisi. Kwa maana ndani ya mioyo ya watu hutoka mawazo mabaya, uasherati, wivi, uuaji, uzinzi, TAMAA MBAYA, ukorofi, hila, ufisadi, kijicho, matukano, kiburi, upumbavu. Haya yote yaliyo maovu yatoka ndani, nayo yamtia mtu unajisi."*** (Mariko 7:20-23).

Kuto kakwa nabii za kimaandiko, tunajua kwamba watu wa nyakati zetu za kisasa bila shaka watateseka kwa ulafi ambao wamejiruhusu wenyewe kuwa wameshikwa nao. Watu wa ulimwengu watalazimika kuvumilia kipindi cha jangwani cha dhiki kuondoa mtazamo wao mbaya na mwenendo katika kuoshwa kwa ulimwengu mzima. Dhiki Kuu itakuwa wakati wa shida ambayo haijawahi kushuhudiwa awali. Sio lazima upitie hukumu hiyo kali kutoka Juu. Unaweza jihukumu sasa, kwa kuendelea, kwa msingi wa siku hadi siku kulingana na Neno la Yahweh, kuiruhusu kukuelekeza kwenye njia za haki, ili kwamba hutalaaniwa pamoja na ulimwengu. Angalia 1 Wakorintho 11:31-32. Utakubali mwaliko huu kutoka kwa Yahweh, Mwenye-nguvu, Baba wa Mbinguni, kutafuta maisha yaliyogeuzwa na kumtumikia Yeye kwa moyo wote? Na Yahweh, kupitia kwa Mwana Wake, Yahshua aliye Messiah, Mwokozi wetu, akupee hamu kumtumikia Yeye katika heshima na uaminifu. Ninakuacha na fikra hii inayopatikana katika Mithali 28:16. ***"Mkuu aliyepungukiwa na akili pia huwaonea watu sana; bali ACHUKIAYE KUTAMANI ATAONGEZA SIKU ZAKE."*** Huu urefu wa siku- maisha marefu- yatatimizwa kabisa kama zawadi katika Ufalme unaokuja wa Yahweh. SNB

*Sacred Name Broadcaster*
*Bethel, PA 19507*

PERIODICAL
Reading, PA

# Vifaa Vyako Bora Zaidi vya Kusoma Biblia




## WMLK Radio

### Assemblies of Yahweh Shortwave

**Now Broadcasting 6 DAYS A WEEK**

**15150 kHz 1200-1700 GMT (7 AM - 12 PM EST)**

**17525 kHz 1730-2230 GMT (12:30 PM - 5:30 PM EST)**

**9275 kHz 2300-0400 GMT (6 PM - 11 PM EST)**

**Hewani masaa 24 kila siku kwa WMLKRadio.com, katika TuneIn.com au Katika station.voscast.com/5cfe89883c143**

(Note: There are times that WMLK is not broadcasting because of maintenance or repairs.)